

Jina ..... Nambari .....

102/2

Sahihi .....

Tarehe .....

**KISWAHILI**

Karatasi ya Pili

(Ufahamu, ufupisho, Sarufi na matumizi ya lugha na Isimujamii)

Julai / Agosti 2016

Muda: Saa 2½

**MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WA NYANDARUA KUSINI**  
**Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya**  
**Kidato cha Nne**

**KISWAHILI**

Karatasi - 102/2

Julai / Agosti 2016

Muda : Saa 2½

**MAAGIZO**

- Andika jina na nambari yako kwenye nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani.
- Jibu maswali yote.
- Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
- Majibu yako yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

**SWALI**      **ALAMA**      **TUZO**

1                  15

15

3                  40

10

**JUMLA**      **80**

## 1. UFAHAMU (alama 15)

### Soma taarifa inayofuata kisha uyajibu maswali

Nyumba ya Ndolo ya vyumba viwili ilikumbwa na hali mbili tofauti usiku huo. Chumbani alimolala Ndolo mwenyewe, kimya cha kaburi kilikatizwa na misono yake. Mara mojamoja alijigeuza kitandani na kuzifanya mbavu za kitand<sup>c</sup> zilalamikie : uzito wake. Katika chumba kingine, misono ya Ndolo na milio ya chenene ilimkirihi Msela. Kuzidisha, mawazo kuhusu hali ya mamake na unyama aliotendewa babake yalimtoroshea usingizi. Akasalia kujilaza kwenye mkeka wake.

Kila alipotafakari ma<sup>n</sup>eno ya mzee Ndolo ndivyo Msela alivyozi kuamini kwamba matatizo ya familia yao yalisababishwa na Mzee Bonga. Lakini yote hayo akayapuuza. Kubwa kwake lilikuwa ni kumwona mama yake na kujua ni hatua gani atakayochukua licha ya uzito aliouona mbele yake kwa kutokuwa na kipato. Msela alijikuta kwenye mtihani mgumu ulioifanya mishipa ya kichwa kusimama na kichwa kumuuma.

Kwa sababu ya maumivu hayo, Msela alijisogeza na kujiegemeza kwenye ukuta. Akawa anatazama iinsi Mungu alikuwa akiufanya muujiza wake ambao alikuwa ameukosa kwa muda. Alifurahi kuliona juu ikipenyeza miale yake kisha kujitokeza na kuangaza dunia. Ingawa macho yake yalifurahia napambazuko hayo, moyo wake ulikuwa na machungu. Akili yake ilikuwa na zigo zito la kutafuta ifumbazi ambao kwa upande wake ilikuwa ni ndoto.

Msela alijiuliza mengi katika nafsi yake. Aliisaili nafsi yake kuhusu hisi za ndugu zake, kuhusu hali ya nama yao aliyesemekana kuwa mwendawazimu, na ikiwa walifahamu hilo. Alitaka kujua alikokula na likolala mamake katika hali yake hiyo. Kila fikira iliyompitikia akiliniilitaka kupasua mishipa ya ichwa chake. 'Ina maana hawaoni au nao wamekuwa na roho ya korosho kama Mzee Bonga?' alijisaili Msela. Katika maswali yote hayo, alikosa majibu isipokuwa kuzidisha maumivu ya kichwa. Isingekuwa wa machozi yaliyompunguzia baadhi ya machungu, labda angegeuka hayawani.

Macho ya Msela yaliyompelewa yamevimbwa, tena mekundu kutokana na ukosefu wa usingizi. Mwili wake nao lione kana kunyong'onyea kwa sababu ya mazunge ya mawazo. Alichukua kikopo kilichochoka cha maji a kunawa uso kisha akaenda kukaa juu ya jiwe. Kibaridi kjlichotokana na mvua iliyokuwa ikinyesha ilimpiga lakini hakujali. Angejali vifaa yeye katika intafaruku wa hali ya mamake?

Ingawa Mzee Ndolo alimwita ndani ili aipishe mvua, Msela alidinda. Badala yake, aliendelea kuuachilia twili wake kuloweshwa na michonyoto ya mvua. Kila alivyozi maisha ya wendawazimu ndivyo toyo ulivyozi kumuuma. Akawa yuajiuliza mama yake aliukosea nini ulimwengu hata apate adhabu e. Halafu fumo lake la mwisho moyoni ni madhara ya mvua na baridi ile kwa mamake. Hana makao, una mavazi mazito, hana chocchote! Alipowazia makazi ya jalalani na majumba mabovu ambayo siku tete amekuwa akiwaona wendawazimu wakifaliwa kwayo, aliachama.

### Aswali

Eleza ukinzani ulio katika nyumba ya Ndolo. (alama 2)

Ni yapi yaliyomkosesha usingizi msela? (alama 3)

c) Kwa nini Msela hakuweza kuibadili hali yake. (alama 4)

.....  
.....  
.....  
.....

d) Taja chanzo cha madhila ya Msela. (alama 1)

.....  
.....  
.....

e) Muujiza wa Mungu unatoa taashira gani kwa hali ya msimulizi? (alama 2)

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

## 2. UFUPISHO (alama 15)

Soma'kifungu kisha ujibu maswali

Upo msemo usemao kuwa kuvunjika kwa mwiko si mwisho wa upishi. Msemo huu unaafiki kabisa ari ya watu wazima wengi ambao licha ya umri wao, wamo mbioni kutafuta elimu ili mbali na kupata nuru, wajiuuge na wasomi wengine katika kuikuza na kuiendeleza jamii. Ni kwa sababu hii ndipo serikali, kwa ushirikiano na mashirika mengi yasiyokuwa ya kiserikali, imekuwa mstari wa mbele kutoa tunu hii kwa wazee ili kukata kiu yao ya elimu.

Watu wengi wa umri wa makamo ambao labda walikosa kumaliza masomo ya kiwango fulani au walikosa kabisa kwenda shulenii kwa sababu mbalimbali, hasa za kifedha, wamekuwa wakiweka elimu kama mojawapo ya majukumu yao ya utuuzima. Hii imekuwa dhahiri hasa baada ya serikali ya Kenya kuanzisha mpango wa elimu bila malipo katika shule za msingi, kwani idadi ya watu wazima ambao warnejitokeza kunufaika na mpango huo haisemeki. Pamoja na mpango huo, wapo wale ambao walikosa cusoma au kumaliza masomo kwa sababu ya karo, na kwa sababu sasa wana mapato, wameazimia cujiendeleza, ili wapate vyeti. Hii ndiyo maana si ajabu kuona hata wafungwa kwenye magereza vakifanya mitihani ya kitaifa.

Elimu ya watu wazima huteklezwa kwa njia mbalimbali. Kunayo elimu ambayo inalenga kuwapa watu awa ujuzi wa kuiendeleza kiuchumi. Kutokana na ufundi wanaofundishwa, ambao huwa ni kazi kama seremala, umekanika, ushoni, usonara na kadhalika, huwawezesha kujitegemea kimapato, kwa hivyo vakaweza kuwapa wanao fursa ya kufaidi kile ambacho wao walikikosa.

unayo pia aina ya elimu ya watu wazima ambayo inaegemea maslahi ya watu hawa, hasa mafunzo

ihiusu afya na usafi, masuala ya kifamilia na mahusiano na pia suala la ulezi. Kwa kufanya hivi, watu iwa hupata motisha ya kutangamana na watu wengine na kubadilishana nao mawazo kuhusu masuala nayoathiri maisha yao Ndiyo sababu utapata watu wa aina hii wana ujuzi mkubwa wa kila kitu nachoendelea katika kila kona ya nchi.

na nyine ya elimu kwa watu wazima ni ile ya umma, inayohusu hasa masuala ya kisiasa. Mara ingi, utawaona wakongwe wakipishwa kwenvye foleni ili kwenda kupiga kura. Hii ni kwa sababu, mbali kuwa huenda wakawa wamestaafu kikazi, bado wana jukumu muhimu sana katika kufanya maamuzi kisiasa kwa ajili ya vizazi vyao. Hivyo basi, serikali hufanya kila juhudini kuhakikisha kuwa hamasisho etolewa kwa kila mwananchi, pamoja na kutoa mafunzo ya namna ya kupiga kura ili kura zisiharibike, sa baada ya mtu kuitia utaratibu mrefu na wenye kuchosha wa kupiga kura. Kwa hili la kisiasa, watu zima wengi hushangaza kwa jinsi wasivyowezwa kushawishika kufanya maamuzi yanayokwenda iyume na maazimio yao.

Eleza masuala muhimu katika aya mbili za kwanza kwa maneno 60.

(alama 7)

Matayarisho

libu

b) Fafanua jinsi elimu ya watu wazima hutekelezwa ukitumia maneno 60. (alama 6)

Matayarisho

## MATUMIZI YA LUGHA. (alama 40)

Taja sifa nne za sauti /a/ (alama 2)

.....  
.....  
.....

- b) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo: (alama 3)

Milangoni

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

- c) Ainisha vitenzi katika sentensi ifutayo. (alama 2)

Wao watakuja kuwa waandishi maarufu.

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

- d) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo. (alama 2)

Huyu amekuja kutuliza.

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

- e) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo. (alama 2)

Mahindi ya mama yamekua kwa kupata myua ya kutosha.

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

- f) Nyambua kitenzi 'chwa' katika kauli ya kutendea kisha ukitungie sentensi. (alama 2)

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

- g) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya neno 'vibaya' kama: (alama 3)

i) Kiyumishi.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

ii) Kielezi.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

iii) Kiwakilishi .....

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

h) Changanua kwa kutumia jedwali. (alama 3)

Yeye alifaulu ingawa hana adabu

.....  
.....  
.....

i) Akifisha sentensi ifuatayo: (alama 2)

Je ni nani alingoa mti wa kiprono

.....  
.....

j) Taja msemo mwingine wenyewe maana sawa na : (alama 1)

piga maji

.....  
.....

k) Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi cha pekee cha kusisitiza katika ngeli ya U/U (alama 2)

.....  
.....

l) Bainisha matumizi ya 'po' katika sentensi ifuatayo. (alama 1)

Alipowasili alionyeshwa walipo

.....  
.....

m) Bainisha matumizi ya 'ni' (alama 2)

Kimbieni! Huyu ni mnyama aliyeniuma mguuni.

.....  
.....

n) Tunga sentensi moja kudhihirisha maana ya vitate rika na lika. (alama 2)

.....  
.....

- o) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo .  
Jane alitengenezewa kiti na fundi kwa nyundo (alama 3)
- .....
- .....
- .....

- p) Unda nomino dhahania kutokana na kitenzi - abudu. (alama 1)
- .....

- q) Tunga sentensi kwa kutumia kivumishi cha sifa kisichoambishika. (alama 2)
- .....
- .....

- r) Andika kwa wingi. (alama 2)
- Seremala huyo alikuula ndizi kwa uma.
- .....

- s) Kanusha sentensi ifuatayo bila kutumia kiunganishi. (alama 2)
- Iwapo mvua itanyesha wakulima watapanda mapema.
- .....

- t) Eleza maana ya kiimbo. (alama 1)
- .....

4. **ISIMUJAMII (alama 10)**  
a) Taja nadharia tatu zinazoelezea chimbuko la lugha ya Kiswahili. (alama 3)
- .....
- .....
- .....
- .....
- .....
- .....
- .....
- .....

b) 'Mkinichagua, mimi tutaimarisha masomo, huduma za afya, barabara na pia maji mtapata hivi karibuni. (makofsi na vigeregere).

- i) Tambua sajili hii (alama 1)

ii) Eleza sifa sita za sajili hii. (alamu 6)